JAMHURI YA MUUNGANO **WA TANZANIA**
OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA
WAKALA YA SERIKALI MTANDAO
Samora, Avenue, ExTelecoms House, 2nd Floor, P.O Box 4273, Dar es Salaam, Tel: +255222129868/74, Fax: +255222129878,
General eMail: info@ega.go.tz, CEO eMail: ceo@ega.go.tz, Website: www.ega.go.tz

Uratibu na Udhibiti wa Miradi ya TEHAMA unapunguza gharama za uendeshaji Serikalini

Na Catherine Peter

Katika mambo yaliyokuwa yanarudisha nyuma matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na kusababisha wananchi kutonufaika na ujio wa teknolojia hii kwa ukamilifu ni kutokana na ukosefu wa uratibu, udhibiti na ushauri wa utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao ndani ya Serikali.

Kutokana na ukosefu huo, kila taasisi ya umma ilijaribu kuanzisha miradi na kusimika mifumo mbalimbali ya TEHAMA bila kupata ushauri wowote iwapo mfumo huo utaweza kujiendesha wenyewe baada ya mradi kukamilika, kwa kuwa hata gharama za uendeshaji wa mifumo hiyo katika baadhi ya taasisi hizo hazikujulikana, na hivyo kuleta changamoto kubwa za uendeshaji wa mifumo hiyo Serikalini.

Hivyo, ili kutatua tatizo hilo pamoja na changamoto mbalimbali zinazohusiana na uratibu, udhibiti na ushauri kuhusu uendeshaji wa Miradi ya TEHAMA Serikalini, Serikali ilianzisha Wakala ya Serikali Mtandao mwaka 2012 na kuipa jukumu na mamlaka ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao ikiwa ni pamoja na Miradi ya TEHAMA Serikalini.

Mkurugenzi wa Udhibiti wa Huduma za Serikali Mtandao, Bw. Michael Moshiro anasema kuwa kabla ya kuanzishwa Wakala hii (2012), kila Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ilikuwa inabuni miradi yake ya TEHAMA ambayo ilikuwa inonekana kurudufiwa kwa kuwa hakukuwa na chombo cha kuratibu miradi hiyo. Hivyo, taasisi za umma zilikuwa zinatumia sehemu ndogo ya miundombinu hiyo mikubwa ambayo ingeweza kutumiwa na taasisi zaidi ya moja.

Maafisa TEHAMA Serikalini wakifuatilia kwa makini mafunzo kuhusu usimamizi wa miradi mbalimbali ya TEHAMA Serikalini.

Bw. Moshiro anasema ili kukabiliana na changamoto hiyo Wakala imeandaa Miongozo, Viwango, Kanuni na Vigezo mbalimbali ambavyo vinatumika katika usimamizi, udhibiti wa miradi au mifumo ya TEHAMA ndani ya taasisi zote za umma. Hivyo, taasisi za umma (Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na taasisi nyingine za umma zinazoanzisha na kuendesha miradi ya TEHAMA au zinazotoa huduma kwa umma kwa njia ya mtandao zinawajibu wa kuhakikisha kuwa Miongozo, Viwango, Kanuni na vigezo hivyo vilivyowekwa vinafuatwa.

Akifafanua zaidi kuhusu vipimo vinavyotumika kusanifisha miradi ya TEHAMA Serikalini, Bw. Moshiro anasema kuwa mradi wowote wa TEHAMA wa taasisi ya umma, bila kujali aina ya taasisi inayoutekeleza ni mali ya Serikali, hivyo lazima miradi hiyo itawaliwe na viwango vinavyokubalika kiserikali. Kipimo kikubwa kinachopima uhalali wa mradi wowote wa TEHAMA Serikalini ni kuona kama shughuli hiyo inachangia kutimiza malengo ya dira ya Taifa.

Aidha, Serikali wakati wote huwa na dira yake, na ni wajibu wa taasisi zake kubuni jitihada au mifumo itakayotimiza malengo ya dira hiyo. Kwa hapa Tanzania, ni Dira ya Maendeleo 2025 inayokusudia kufanya nchi kuwa na maendeleo yasiyoepukika ili kufikia hadhi ya pato la kati; ikiwa na viwanda vya kisasa zaidi, ushindani, maisha bora, utawala wa sheria na kuwa na jamii iliyoelimika na inayopenda kusoma. Anasema Bw. Moshiro.

Bw. Moshiro anaendelea kueleza kuwa kipimo kingine katika kusanifisha mradi wowote wa TEHAMA Serikalini, ni kulinda mahitaji ya Serikali ya kulinda usalama na faragha ya taarifa zake.

Vilevile, urahisishaji wa michakato ya utekelezaji wa shughuli za serikali ni moja kati ya vipimo vinavyozingatiwa katika kusanifisha mradi wowote ule. Hivyo, TEHAMA haina budi kufanya maisha kuwa rahisi zaidi kwa kufanya huduma inayotolewa kuwa ya gharama nafuu, inayochukua muda mfupi kuipata bila usumbufu, bila rushwa, inayopatikana wakati wowote na isiyobagua. Kwa upande wa Serikali yenyewe, utoaji wa huduma hiyo nao uwe wa gharama nafuu wakati huo huo ikiwezesha serikali kupata mapato. Anafafanua Bw. Moshiro.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Programu za TEHAMA Bw. Laizer Nassor anasema kuwa miradi mingi ya TEHAMA iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji tayari imepewa ushauri na msaada wa namna moja au nyingine na Wakala. Mradi wa TEHAMA wowote unaowasilishwa kwa Wakala hufanyiwa uhakiki kwa kutumia vigezo mbalimbali. Anasema Bw. Nassor

Akifafanua vigezo hivyo, Bw. Nasoor anasema kigezo cha kwanza ni kuhahiki dhana ya mradi kama inaendana na malengo ya Serikali, unazingatia Dira na Dhana ya taasisi husika, umuhimu wa mradi huo kwa taasisi husika na kuona kama unaendana na Sera, Viwango, Miongozo na Taratibu za Serikali.

Kigezo cha pili ni kuhakiki kama mradi unaokusudiwa kutekelezwa unaboresha mchakato wa utoaji huduma kwa umma na watumiaji wanaona jinsi TEHAMA inavyorahisisha utaratibu wa upatikanaji wa huduma husika wakilinganisha na utaratibu wa zamani. Kigezo cha tatu ni kuhakiki kama mradi umeshirikisha maoni

ya wadau na umemilikiwa na watekelezaji wa mradi huo kama mali yao na kujihusisha kwa undani zaidi na kuona fahari kutekeleza mradi huo. Anasema Bw. Nassor.

Bw. Nassor anataja kigezo cha nne ni kuhakiki uhusiano uliopo kati ya jitihada hiyo na nyingine za aina hiyo zinazotekelezwa katika taasisi za umma. Hii inasaidia kuondoa urudufu na kutoa fursa ya kushirikiana vifaa mbalimbali na hivyo kupunguza gharama, wakati kigezo cha tano ni aina na mtindo wa teknolojia inayotumika, kama ni rafiki kwa watumiaji na ni endelevu, kwa maana ya kuweza kuisimamia na kuiendeleza.

Vilevile Bw. Nassor anasema kigezo cha sita ambacho ni muhimu ni muda katika utekelezaji wa mradi wa TEHAMA kwani ucheleweshaji unaweza kusababisha teknolojia inayohusika kupitwa na wakati, mahitaji ya wateja kubadilika au hata kupanda kwa gharama kwa vifaa mbalimbali zinazotumika.

Kutokana na uzoefu, miradi mingi inashindwa kutimiza malengo kutokana na kushindwa kuendelea baada ya uwekezaji kukamilika. Hivyo, Bw. Nassor anasema kigezo cha saba ni kuzingatia uwezo wa mradi kujitegemea au kushindwa kubuni utaratibu utakaohakikisha kuwa mradi huo unakuwa endelevu na ni lazima jambo hili libainishwe toka mwanzo wakati wa kubuni mradi. Anasema Bw. Laizer

Lazier anazidi kuelezea kwakusema kuwa kigezo cha nane ni uzingatiwaji wa masuala ya fedha kwa kuangalia kama vyanzo vyote na gharama ya mradi vimebainishwa na gharama za uendeshaji wa mradi huo zimeonyeshwa wazi na kigezo cha tisa ni Usimamizi wa Dharura ambapo hilo ni jambo la muhimu kulizingatia kwa kuhakikisha kuwa masuala ya dharura yanayoweza kujitoleza kwenye mradi huo wa TEHAMA yamebainishwa.

Laizer anasema, baada ya kuhakiki, iwapo mradi huo umekidhi vigezo vyote mradi huo hushauriwa kuendelea na kama haukukidhi hushauriwa kuachwa na badala yake ubuniwe mwingine.

Kutokana na vigezo hivyo, Wakala inashauri kila taasisi ya umma ishirikiane na Wakala ili iweze kupata ushauri wa kitaalamu kabla ya kabla kupanga na kuanzisha mradi wowote wa TEHAMA kama ilivyoelekezwa katika Mwongozo wa Matumizi Bora, Sahihi, na Salama ya Vifaa na Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Serikalini wa mwaka 2012 na Waraka Na. 3 wa Mkuu wa utumishi wa Umma wa mwaka 2013 unaohusu uratibu na utekelexzaji wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA katika utumishi wa umma.

Naye Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Angella Kairuki (mb) alipotembelea Ofisi za Wakala mwishoni mwa mwezi Desemba mwaka 2015, aliziagiza taasisi za umma kushirikiana na Wakala katika hatua zote za utekelezaji wa miradi ya TEHAMA hususan wakati wa kubuni na kutekeleza miradi ili Wakala iweze kutoa ushauri wa kitaalamu na Kupunguza gharama za uendeshaji kwa Kupunguza urudufu wa miradi ya TEHAMA

Ni dhahiri kuwa iwapo taasisi zote za umma zitafuata vigezo vilivyoainishwa katika orodha hakiki hiyo, urudufu wa miradi ya TEHAMA itapungua, mifumo ya taasisi hizo nayo itakuwa na uwezo wa kubadilisha taarifa hivyo kuongeza ufanisi mkubwa katika utendaji kazi na kutoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha

gharama za uwezeshaji zitapungua na mapato yataongezeka kwa kuwa mifumo itakuwa salama zaidi na inaanzishwa kulingana na mahitaji ya wananchi na si kwa shinikizo la wafadhili.

Hivyo ni vyema taasisi za umma zikashirikiana na wakala katika kutimiza azima hiyo pamoja na kufuata miongozo na taratibu mbalimbali zilizowekwa katika kuhakikisha miradi ya TEHAMA inayoanzisha inaleta tija na inalenga kufikia malengo ya dira ya taifa ya 2025.